

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

[Redacted]

[Redacted]

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

KITUI WEST CONTITUENCY HELT AT

A.I.C. KIAYINE, MATINYANI

[Redacted]

[Redacted]

[Redacted]

[Redacted]

ON

[Redacted]

[Redacted]



4 JUNE 2002

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, KITUI WEST CONSTITUENCY, HELT AT A.I.C. KIAYINE,

MATINYANI ON 4TH JUNE 2002

Present

Com. Pastor Zablon Ayonga
Com. P.M. Wambua
Com. Charles maranga

Secretariat in Attendance

Collins Mukewa - Programme Officer
Elizabeth Nderitu - Assistant Programme Officer
Zipporah Wambua - Verbatim Recorder

The meeting started at 9.45 a.m. with Commissioner Wambua in the Chair.

Speaker: Hawa wako nje ya compound waanze kuingia.

Com. Wambua: Everyone understands, kama ni Wakamba nitaongea Kikamba wale ambao sio Wakamba tutafanya translation, wacha kwanza nianze na Kizungu.

Mabibi na mabwana tungelipenda kuanza kikao hiki. Hapa tuko na Commissioners watatu, ningelipenda kuwajulisha wale ambao wamefika leo. Kwanza tuko na Pastor Zablon Fena Ayonga, ni mzee ambaye ndiye anawakilisha wale ambao mnaita Senior Citizens. Mzee ndiye anatuonyesha njia huko kwa Commission, amefanya kazi na Kanisa la SDA kwa miaka mingi, karibu 30 ama zaidi. Hapa tuko na Commissioner Dr. Charles Maranga Bagwasi, Charles Maranga ni mtu anayejulikana sana, amesomesha huko Kenyatta University miaka mingi na pia wakati moja akajaribu siasa, aka-retire, akaingia kwa Commission, amesema pengine wakati ujao pengine atajaribu kuuliza hiyo kazi tena, kwa hivyo tunataka kumpatia maombi. Mimi kwa upande wangu nafikiria mnanijua, mimi ni mtu wenu hapa, natoka hapa hapa tu. Sijui kama mnataka majina. Paul Musili Wambua Commissioner.

Upande huu tuko na Secretariat Staff, wale ambao tumekuja na wao ndio watatusaidia. Kwanza tuko na Collins Mukewa ndio huyu hapo, yeye ni Programme Officer huko kwa Commission. Tuko na Elizabeth Nderitu, Assistant Programme Officer – Commission na tuko na Zipporah Wambua, but not related with me yeye ni mtu wa kutoka uko Matuu, lakini she is also a Verbatim Recorder, sitaki msemu nilikuja na sister yangu. Yeye ni verbatim recorder kutoka Commission, so she is the one who is going to record what we are going to say. Halafu nitampatia huyu atasema maanake tuko na Coordinator hapa pia ni

mtu watu, Field Officer, Elizabeth Mumbi mnajua sana na Assistant wake anaitwa Dennis. Those are the Commission officials.

Kwa hivyo Elizabeth itatujulisha 3C's tumalize this programme maanake sasa uko mwisho mwisho pengine hatutakuwa na wakati. Utuonyeshe members wa 3C's wale wa Kitui West halafu nitampatia nafasi Dr. Charles Marange ambaye atakuwa ndiye Mwenyekiti wa kikao hiki aendeshe sasa, kuanzia sasa. Kwa hivyo Elizabeth utujulisha watu wako, nawajua wote mimi lakini nafikiria ma-Commissioners wangependa kuwaona. Wao wamesikia mnafanya kazi vizuri lakini hawajui ni akina nani, kwa hivyo tafadhali utujulisha members of the Constituency Committee.

Elizabeth Mumbi: Kwanza wacha tuanze kwa maombi, ningependa kumwalika Malusi. Ningependa kumwalika Mr. Malusi atufungulie mkutano wetu kwa maombi. Karibu.

Mr. Malusi: Tuombeni. Baba katika jina la Yesu twaja mbele zako kwa unyenyekevu, tukijua na kukubali ya kwamba bila wewe, hatuwezi chochote. Tuna kile ambacho kimesababisha tukusanyike hapa, tunataka hekima, tunahitaji pia maarifa hayo hatuna ila wewe utuongoze, twaomba roho wako na uwepo wako uwe nasi, uanze nasi, uendelee nasi na umalize nasi. Yale ambao tutatenda katika jumu hili yawe ya kulitukuza jina lako na yawe ya manufaa kwa nchi yetu ya Kenya. Twaombea serikali na wale wanaoiongoza, President na Mawaziri na Wabunge na Madiwani na wafanyikazi wote wa serikali wa Local Authority na yeyote yule ambaye anahuduku kwa mambo yote, pia twakumbuka wahudumu wa kazi yako wachungaji na wote ambao wanaeneza injili yako ili kuwoko amani na utulivu katika nchi.

Twaomba baba utusamehe kwa yote ambao tumekukosa kwa mafikira, kwa maneno na kwa matendo na twaomba uongozi wako. Uwe nasi, uwe na Mwenyekiti, uwe na hao wengine Wanatumia and wale wote ambao wanasaidiana nao na sisi zote, ili tusije tukachukua mafikira yetu tukapeleka mbali na kusudi yetu itakuwa wakati huu. Uwe nasi, utuongoze, utubariki na katika jina la Yesu Christo, mwokozi na mwongozi wetu tunaomba. Amina.

Elizabeth Mumbi: Wacha nichukue fursa hii niulize wanakamati wote wasimame ili niweze kuwajulisha kwa wageni na wale wengine. Hapa tuko na Jeremiah Mulu, huyu ndie Chairman wa Kitui West Constituency. Halafu mbele yake kuko na Penina Kimanzi pia na mwanakamati, mbele yake kuko na Bibiana Mulwa – Member na tuko na Fred Mwalimu, mbele yake kuko na Francis Ndingu, huyu ndie Vice Chairman. Wale wengine hawajafika lakini walikuwa wakitoka mbali sana, watafika pia tutakuwa na wao na ningependa kuwajulisha yule amekuwa akifunza Location hii. Mr. Malusi, amekuwa mwalimu wa Civic Education katika hii Location.

Kwa hayo wacha niridisha kwa (sentence incomplete)

Com. Wambua: Nienda kunena kimusye nikenda withiwe niatkwatania. Ndinegiwe mwantha usu ninge? Tutisye mwantha

uu nieundu wa kwithiwa ni mwise undu koo twikalaa na tuikwenda mundu asye nutatililwe, avatwa mwanth wa kunengane views syake. Kwoudo twenda wise kwithiwa kila mundu ni wakwata mwantha, na twanenea kavati nitwendie twathukuma undu twaiwane na twanengwa mwantha uu. Na niasya andu ala manahusika na wia wa kuvanga akina Mulu na Coordinator ni mutavisye andu withiwe ni mooka, nikenda withiwe ni maumya maoni moo. Tuikwendaa mwongela ngewa nundu ni twisena twenda kumya mwantha kwa kila mundu withiwe niwatugenga maoni moo Na ithye nitookie nikena withiwe nitwatavwa kila undu andu makwasya yulu wa Katiba undu makwenda maandike. Twikatweke vee andu twatiye nza. Na niasya nienda kuvkya ngewa isu vau nundu vaie maana ma kwongela, nitwelailwe.

Kwa hivyo nafikiria madam Coordinator, tuko na area Chief ambaye yuko hapa pengine, one of the unique things about Matinyani is that we always here lady leaders, lady Cabinet Ministers, that is the area Chief, she is Annet Mbiti – Chief Matinyani, nafikiria nimeomwona Chief Mutundu, Cosmas pia yuko pale. He is my Chief actually although I am at the border, I do not know which area I belong to both of them claim that I am their subject because I am at the border. Kwa hivyo nafikiria sasa nitampatia nafasi Commissioner Charles Maranga aendeshe, maana tumepata watu wa kutosha yeye sasa ndiye atatuambia vile tutaendesha mpango wa leo. Thank you.

Com. Maranga: Basi kwanza kabisa nataka kutoa salamu zangu kwa niaba ya Tume ya Kurekebisha Katiba ingawa Commissioner Wambua ameongea, unajua huyu ni mtoto wa nyumbani na mtoto wa nyumbani hana ile maneno wato wanamtambua, wanamwona tu, huyu ni kijana wa fulani hapa. Hakuna maneno mingi, lakini sasa sisi wengine ni wageni hapa na tunataka kusema asante kwa kutukaribisha hapa Matinyani na leo tunataka mtoe maoni yenu bila wasiwasi, ukiwa mfanyi kazi wa serikali kama Chief's na kila mtu, unahaki ya kutoa maoni mbele ya Tume ya Kurekebisha Katiba.

Kwa hivyo Chief's, mahali zingine zote tumeenda hapa nchini Kenya, kama jani nilikuwa Saikuru na District Officer alitoa maoni yake kabisa bila wasiwasi, Chief's walitoa maoni, na kila mahali yote hapa tumeenda Chief's D.O's hata yeyote, awe D.C. hata uliona President mwenyewe anasema anangojea Yash Pal Gai, tuende tuchukue maoni yake, kwa hivyo hata Rais anatoa maoni yake. Tunasikiza hayo maneno? Kwa hivyo mtu asikuambie eti wewe ni mfanyikazi wa serikali uwezi kutoa maoni, unatoa, ukiwa mwalimu, ukiwa nini unatoa maoni yako.

Sasa lakini, kabla hatujaanza, tusikizane ile masharti. Ya kwaza kabisa tutafuata list, kuna list tunajaza hapo nje, ukiingia wewe utaamua kama unakuja kuongea ama utaki kuongea. Kama unataka kuongea basi utajiandikisha na utuambie unaongea ama unapeana memoranda, kuna wengine nakatoa, ama ile memorandum wameandika bila hata kutaka kuongea, kwa hivyo unaweza ukafanya hivyo. Bila kuongea na utoe memorandum yako. Vile vile unaweza kuja hapa, uketi kimya usikize vile wengine wanaongea na vile vile inakubaliwa.

Unaweza kuja hapa unataka kuongea, sasa wale ambao wanataka kuongea ndio ninataka kuwambie zile njia ambazo tunafuata.

Ya kwanza kabisa, mtu anajitambulisha jina lake. La pili, unakubaliwa kuongea lugha yoyote, unaweza kuongea lugha ya Kiswahili, lugha ya Kiingereza ama lugha ya mama. Kwa mfano sasa tuko Matinyani, unaweza kuongea lugha ya Kikamba lakini hata kama hata kuna Mjalu hapa, anaweza kuongea Kijaluo. Tunaelewana hivyo? Kwa hivyo inakubalika.

Tena kitu ingine ya muhimu sana, tunataka mutoe mapendekezo vile unavyotaka, lakini ukitambia. Kwa mfano, ukituambia watu wa Ukambani, taabu zao ni maji, maji, ni maji na hutupi pendekezo vile unataka tufanye, Katiba mpya haitusaidii. Ukisema barabara ni mbaya kati ya Kitui na Mwingi, sasa wewe unatakiwa utupe pendekezo useme, tunataka barabara mzui namna hii, namna hii. Kama ni elimu ni hivyo hivyo, kama ni maneno ya uongozi, ni hivyo hivyo. Kama unataka Chifu waendeleo, utaambie vipi? Kama hutaki waendeleo, utuambie vipi? Tunaelewana? Kwa hivyo mkija mnatoa maoni ile sawasawa.

Tena kitu ingine ni, kuusu muda. Sisi kama Tume ya Kurekebisha Katiba, tumepita mahali mingi hapa nchini Kenya, tumeenda Mkoa wa Pwani, Mkoa wa Mashariki, Mkoa wa North Eastern, huko Nairobi. Tunampa mwananchi dakika 5, ata kama umeandika memorandum, unatupa maoni yako ya muhimu. Ingingine yote, sisi tutaenda kusoma, kama unaongea vile vile tunakupa dakika 5, kwa hivyo unajipanga vilivyo ile maoni ambayo unataka kutoa, uhakikishe kwa hiyo muda umefanya nini? Umetoa. Kwa sababu tunataka kumpa kila mtu nafasi, atoe maoni yake. Tunaelewana? Kwa hivyo hiyo ndio wakati, kwa hivyo mimi kama Chairman, sitakuwa naongea, nikiona wewe unazidi, nakuambia sasa malizia ama nitakukata. Tunaelewana? Lakini sitaka ufike wakati huo, mimi nataka unatoa maoni yako kwa wakati ambayo tumekubaliana. Tunaelewana kwa hiyo maneno?

La mwisho kabisa mtu akitoa maoni yake ata kama unakubaliana naye, hukubaliani naye, hiyo ni maoni yake. Sisi hapa hatusemi, haa, hatusemi tushangilie huyu ama nini! Hapa sio mkutano wa siasa, mtu anatoa maoni vile unataka. Tumekubaliana? Kwa hivyo mimi sasa, naambiwa wale ambao wako na simu ya mkono ile inaitwa mobile, ile simu ambaye inatembea kila mahali, kama Coordinator mimi najua ako na moja. Mnazima zote kwa sababu inafanya hitilafu kwa mitambo ya kunasia sauti zenu. Kwa hivyo hayo ndio nafikiri nitasema. Com. Wambua.

(Interjection)

Kwa hivyo, ukimaliza kuongea hapa mbele yetu, kuna kijitabu huko, register rasmi ya Tume ya Kurekebisha Katiba, utaenda huko uweke sahihi, utuwachie memorandum, ata kama huna memorandum, utaweka sahihi ya kuonyesha kuwa umefika mbele ya Tumbe ya Kurekebisha Katiba na hiyo ni recordi ya kihistoria, itakuweco na itaendelea kuwa hapo. Hiyo ni permanent record ya Commission.

Ata ukioni Commissioners hapa hawaandiki kila kitu, wanachukua point fulani, tunanasa sauti yenu yote. Ata kama ukikohoa

wakati unaongea tutaanasa hiyo kukohoa. Unasikia hivyo? Kwa hivyo kila kitu iko recorded. Tunaelewana? Kwa sababu kuna wazee wengine wakiona Commissioners hawaandiki, wanasema mnasekiza maneno yangu kweli? Kwa nini hamwandiki? Tunanasa huko record yenu. Tunauliza hiyo jina yenu kwa sababu wakati tutakuja kuleta report unataka kusoma. Naweza kusema, Elizabeth Samuel, aliongea nini? Mulwa aliongea nini? Fulani aliongea nin? Annet aliongea nini? Tunaelewana? Kwa hivyo hiyo ni maneno ya muhimu.

Basi bila kupoteza wakati, sasa ni saa nne kasoro dakika saba tunaanza mkutano wetu rasmi wa kuanza kusikiza maoni na yule ambaye anatoa maoni, utakaa hapa, tutakuwa na mic hapa. Unakuja unaketi hapa halafu unatoa maoni yako.

Kwa hivyo wa kwanza kabisa ni Councillor Musyimi Manzi.

Coun. Musyimi: I am Councillor Joseph Musyimi. I will represent my views towards the Constitution Review.

I suggest that Councilors should get their salaries from the Central Government.

They are elected members of the Council, like the elected Members of Parliament and so, they should draw their salaries from the Central Government. The Councilors conduct a lot of Harambee in their areas and meet all sorts of demands from the people of their areas in developing their areas.

I suggest that their salaries be increased to Kshs. 50,000/= or Kshs. 100,000/= per month so as to meet the areas demand. I also suggest that, any Councilors elected in the Council for 1 term of 5 years, he or she should qualify for pension.

I suggest that ballot papers cast at any polling station should be counted at the same polling station, and the Presiding Officer of the Polling Station carry announce the result to a central point, where the results from all other Polling Stations shall be counted.

The idea of carrying ballot boxes to the central counting point has been noted as cheating is concerned.

Political Party: Political parties should be 3 only, there is no need for many political parties in this country, if we want to develop the country.

Thank you.

Com. Maranga: Ngoja kidogo, kitu ambayo sikuwaelezea kabla pengine haujatoka kwa kiti ya maoni saa ingine Commissioners wangetaka kukuuliza maswali ama kuakikisha ya kua ile maoni umetoa ameyasikia kwa usawa, kwa hivyo nitauliza Commissioners wenzangu kama wana swali na kama hawani utamalizia hapa. Any questions? No. O.K.

Thank you very much sasa Councillor uende uko uweke sahihi kwa huyo kijana chipukizi huyu, uweke sahihi mbale yake huyo anaitwa bwana Mukewe.

(Interjection)

Com. Maranga: No, it is O.K., we are all right there is no problem.

The next one is Permenas Munyanya, Munyasia sorry and my apologies.

Parmenas Munyasia: Mr. Chairman, Sir, My name is Honorable Parmenas Nzilu Munyasia and I am just presenting my memorandum towards Constitution Review.

Mr. Chairman Sir, the first thing is extension of time concerning your Commissioner.

1. Mr. Chairman Sir, my view is that the Commission should be give sufficient time to produce a comprehensive Constitution to avoid sooner amendments if elections were to be held this year using the old Constitution. That is my view number one.

2. National ceremonies: Mr. Chairman Sir, the Commission must remember that the Kenyatta day to my view, was wrongly considered and my view is, Kenyatta Day is called Kenyatta day because Kenyatta and the other 5 persons were detained on the 20th October 1952, same day, same night, same year and therefore only 6 people were ddetained on that particular day and therefore others were sooner detained and sent to other detentions. Therefore my proposal is, that the Kenyatta Day should be scratched off, to pave way for those who were detained together with Kenyatta on 20th October 1952 and are still alive to deliver speeches to the nation as on that material day.

Mr. Chairman Sir, I will quote afew who are alive and those who are dead. The Honorable Jomo Kenyatta is dead, the Honorable Kungu Karumba is dead, the Honorable Benard Kubai is dead. Those alive are Joseph Paul Ngei, Honorable Ochieng' Oneko, Honorable Kaggia, those are still alive and they should deliver speeches, so that the younger generations should understand how the few fought for independence.

Latter on others were detained in a massive way, Mau Mau leaders and leaders of various groups and other organizations and therefore, the Review Commission should consider that very seriously. When I was giving a comprehensive report on the questionnaire book or document, I left one word about the Police Force.

3. The Police Force should be recruited to tally with the Kenya Armed Forces i.e. employed on contract basis of 9 years and later if the 9 years are competed, to reapply for the contract. This will reduce massive corruption, which is currently on, in the

Police Force, and any officer would be careful to perform his duties well knowing that after 9 years contract, if I did not perform well I will be sacked.

4. **Parliamentarians Pension:** My friends of Parliament did not consider seriously where the scheme should begin. They come to those who were sitting in 1998, they said 2 terms of 5 years of their current time. So, after 10 years some had gone out and they were pensionable. Those who come in, 1997 changed that scheme, they said No it is 5 years only. Those members of the current sitting Members of Parliament of 1997 whose time is ending this year, after being thrown out they will qualify, after serving for 5 years.

Your friend said I quote myself, I have done 18 and half years in Parliament 1963 to 1984. I was removed through a petition and I am not pensionable. Therefore, I will say it should read that any person or persons who had been a Member of Parliament since independence (1963) and that he had fulfilled all the requirements as laid down in Parliament Standing Orders should be pensionable.

5. Lastly, Sir in Ukambani we have natural rivers especially Athi River. This river is running through out or along the Ukambani areas to the Sea, after that the water is a waste. This river should be blocked as it was done with Tana River. Tana River, they have got 7 folks but Athi River has none, why that difference? Therefore, when God created the 2 big rivers, he had a purpose for Tana River and Athi River in Ukambani. Why are we skipped off, this is very unfair and therefore, this river should be blocked to allow people to irrigate from both sides and prevent wastage of water running to the sea to be useful, to be utilized for better farming and better use. Thank you Sir.

Com. Maranga: Thank you very much. I think Honorable Parmenas Munyasia, you have a number of questions from the Commissioners and points of clarification.

Com. Wambua: Honorable Munyasia, I would like to know from you whether you have any suggestion regarding the date. You have said that we should scrap Kenyatta Day and you have said that those who are alive and are freedom fighters who were jailed with Kenyatta should deliver speeches. Do you have a proposal as to what name we should give to this holiday? If we should have one or are you suggesting that there should be no holiday to remember those who were arrested on that day?

Hon. Munyasia: Thank you. There is no change for the day, it should remain the same day 20th of October 1952 for heroes, it should be called Heroes Day as done in COTU.

Com. Maranga: There is another question from Pastor Yonga.

Com. Pastor Yonga: My question had been asked by Commissioner Wambua but in addition to that question you said, we

have some of these freedom fighters who are remaining, 3 of them. Now, if these 3 are going to give speeches, what happens to the day, you know as we get old we will die out, after then what happens to that day? Did you take some thought about the continuation of that heroes day, who is now going to speak on their behalf?

Hon. Munyasia: Thank you Sir, I did not say, I think I said specifically that the 3 are still alive but there other groups who are still, the present leaders of Mau Mau who are still alive and other organization leaders because, during the colonial day, they picked the detained leaders. I was detained for 3 months and put in until they could not prove whether I took the Mau Mau Oath.

Com. Maranga: May be the last question from the Chair. What is your position about Nominated Members of Parliament since 1963 to date, do you want them to be considered as elected Members of Parliament?

Hon. Munyasia: Yes.

Com. Maranga: Thank you.

You can now sign our official register with the young man Mr. Collins Mukewa. Thank you very much. Now, the next person is William Kisuzu.

William Kizuzu: Jina langu ni William Kaindulu Kisunzu, kutoka katika Location ya Kalimani na Sub-Location ni Chamzia. Mimi ninakikundi changu cha wazee ambayo tunajiita Chamzia Wazee Self Help Group. Kazi yetu ni kulima, kupanda mboga na kutengeneza matoari ya kuuza ili kupunguza umaskini. Ninatoa shukrani kwa kupewa nafasi hii ili kutoa maoni ya wazee wenzangu.

1. Tumeona sisi raia tupewe nafasi ya kuwachagua ma-Chiefs kwa sababu ma-Chifu ambao wameandikwa siku hizi wanaandikwa kisiasa. Either mwanasiasa anasindikisha mtu yake ndiye anaandikwa Chief. Huyo Chifu hawezi kutumikia raia kwa njia inayofaa kwa sababu ameandikwa na mtu fulani. Wanasiasi ni watu kuchaguliwa na mkundi na kunakuwa na upinzani fulani, kwa hivyo Chief atakuwa akikaa tu kama yule ambaye amemfanya aandikwe, hawezi kutumikia raia kwa njia inayofaa. Kwa hivyo tukipewa nafasi, sisi kuwachagua Machifu nafikiri tutachagua mtu ambaye atatumikia kwa njia inayofaa. Hiyo ni maoni ya kwanza.

2. Katika Katiba ya 1963, wafanyikazi wa serikali walikuwa hawakubaliwi kufanya biashara lakini Katiba imelgezwa wafanyi kazi wa serikali wanafanya biashara, kwa hivyo hawawezi kutumikia raia kwa njia inayofaa na ndio wamefanya uchumu wa nchi kuzoroteka kwa sababu ya ufisadi, kwa hivyo mimi natoa maoni yangu ya kwamba wafanyi kazi wa serikali wasikubaliwe kabisa kufanya biashara. Kama ni kufanya biashara wafanye indirect, wafanye kwa wanawake wao ama watoto wao, lakini

hao wenyewe wakae maofisini watumikie raia kwa njia inayofaa.

3. Naongea juu ya wazee ambao wako zaidi ya miaka 60 kama mimi. Wazee hawa wakifika miaka hiyo, hawatunzwi kwa njia inayofaa na watoto ama wake zao. Kwa hivyo ningepuliza Katiba ya leo ambayo tunatengeneza, ishugulikie wazee. Mimi nimekuwa nikiona wazee Wakizungu wakiwekwa katika Ma-hostels na wanalindwa hapo wanaletewa chakula, wanalishwa vizuri, nguo zao zinafuliwa na wanakaa kwa njia nzuri na wanaishi maisha marefu. Lakini wazee wa siku hizo sisi tunawachiliwa, hatuli vizuri, hatutunzwi vizuri, tunakufa kabla miaka yetu, maisha ambayo Mungu ametuwekea kufika. Kwa hivyo ninauliza Commission hii itutengenezee Katiba ambayo wazee watalindwa na serikali.

4. Maoni yangu ya mwisho, kuna wazee wanaoitwa Village Elders. Hawa wazee wanaitwa Village Elders wanafanya kazi nyingi hata kuliko Assistants Chiefs ambao wako chini wao. Wanaleta amani katika village kwa kuamua mambo mengi, watoto wamepigana huko, akina mama wametukanana, mbuzi imekula shamba la mtu, hayo yote yanaletwe kwa hao wazee wa Village Elders na wanaamua. Kwa hivyo amani nyingi ambayo iko katika nchi inaanzia kwa wazee halafu inaenda juu. Kwa hivyo hawa wazee hawalipwi chochote, mimi ningepuliza Katiba ikitengenezwa, kwa sababu ni yetu, wazee hawa wa Village Elders walipwe. Kwa sababu katika Kenya hakuna mtu anatakiwa kufanya kazi bure, walipwe na hiyo ni njia moja ya kupunguza umaskini. Kwa hivyo maoni yangu inakwamia hapo. Asante.

Com. Marange: Asante Mzee William. Kuna swali?

Com. Pastor Ayonga: Mzee William umesema wazee wawekwe katika ma-hostels. Mtu akifika miaka 60, weka hostel. Ndivyo ambavyo ulisema? Ili alishwe na anaweza kukaa siku nyingi kwa maana hivyo ndivyo Wazungu wanafanya, ndivyo imesema?

William Kisuzu: Ndio nimesema hivyo.

Com. Pastor Ayonga: Mzee ufikiri kwamba, kuenda kuweka wazee katika ma-hosteli ni kama kuweka wazee gerezani. Hiyo ni detention na wazee hawa si wana watoto na wana wajukuu na wazee hawa wanapenda kuishi katika community. Hujui kiwemo katika Community inakufanya usikie uko appreciated by people. Lakini sasa detention hii mambo leo ya kuweka wazee wafungiwe, walishwe na kuwasafishia nguo. Unafikiri wazee wa Kikamba watapenda mambo kama hiyo? Au watoto wa hawa wazee, baba yako akifika miaka 60, anachukuliwa anafungiwa kwa hostel. Hii maneno unaona itapendeza Wakamba au na Waafrika wote wa Kenya?

Mzee William: Mimi nafikiria hiyo inafaa na tumeona na wazee wenzangu kama inafaa.

Com. Pastor Ayonga: Basi hayo tuyaache ni maoni yako lakini mimi nisingependa.

Com. Maranga: Unajua wazee wawili wakizozana hatutaki kuingilia. Basi asante Bwana William, uweke sahihi. Ngojea kidogo Commissioner Wambua inaonekana ana swali kwako.

Com. Wambua: Kuna kitu umesema na nimejaribu kufikiria lakini naona sielewi. Ni kama umesema public servants, wale wafanyikazi wa serikali wasiruhusiwe kufanya biashara lakini ukasema pengine waruusu watoto wao, mabibi zao wafanye biashara. Je, unasema kwamba kama mtu ni District Commissioner ama mtu anafanya kazi kama officer wa serikali, anaweza kuweka biashara yake, lakini badala yake kuendesha hiyo biashara anaweka bibi yake. Si, ile lengo ambayo tulikuwa tunataka ya kuakikisha kwamba hatumii cheo chake, pahali anapofanya kazi kuakikisha kwamba anajifaidisha, hakitazuilika ikiwa tutaruhusu bibi ama mtoto wake aendeshe biashara kwa niaba yake? Sijui kama umenielewa? Umenielewa?

Mzee William: Sielewi vizuri.

Com. Wambua: Umesema mtu kama ni public servant ama anafanya kazi asirusiwe kufanya biashara lakini mtoto wake na bibi yake wanaweza kurusiwa. Si hiyo itakuwa, ile jambo ambalo tunataka kumaliza ya huyo bwana kutumia cheo chake, kuakikisha kwamba amejifaidisha, kitakuwa tu atujakizua kabisa manake anaweza kufanya hiyo biashara kwa jina ya bibi yake ama mtoto wake?

Mzee William: Hapo ninaeleza ya kwamba akifanya kazi in-direct, yaani watu wake kama bibi ama mtoto akifanya biashara atakuwa akiwaangalia tu lakini awe hayuko ndani.

Com. Maranga: Asante mzee wangu weka sahihi kitabu chetu rasmi hiyo itakuwa mzuri kwetu. Mwingine ni Kivunza mboti. Lakini kabla hapo vile anavyokuja, ningependa kumtambua His Worship the Mayor of Kitui Municipality, Councillor Julius Kaango, umekaribishwa nafikiri utapeana maoni kuusu Local Authorities. Asante.

Kivunza Mboti: Mimi naitwa Kivunza Mboti kutoka Matunyani Location, Kalya Sub-Location.

Maoni yangu ni kama haya, tumepata Land Survey in 1971 ndio ilingia Matinyani, 1971, 1972 na 1973 tukapata title deed la shamba letu, tulikuwa tunachukua title deed na Shilling 50/=, tulichukua lakini hawakuchukua sababu hawana Shilingi 50/=. Kutoka 1971 hata sasa title deed ni sawa, kikundi cha Matinyani Location tunaambiwa ofisi Kitui kwa ajili ya pesa. Title deed yangu ifanywe Sub-division ndio wagawiwe shamba, kila shamba naitishwa 6,000/= ili mtoto wangu afanyiwe sub-division kwa shamba langu na nilichukua title deed na Shilling 50/= in 1971 na 1972.

Com. Wambua: Hiyo pesa ambayo wanaitisha ni pesa ambayo inatakikana ilipwe na serikali ambayo ni pesa inatakikana iende kwa mifuko ya watu?

Mzee Mboti: Survey fees

Com. Wambua: Endelea.

Mzee Mboti: Sasa mimi nataka gawia watoto wangu shamba na sina hiyo pesa ya kupeleka kwa survey na niko na title deed. Kikundi cha Matinyani Location, title deed yao imekwama ofisini kwa ajili ya pesa.

Com. Wambua: Haya utuambie unataka nini.

Mzee Mboti: Haya ndio maoni yangu.

Com. Wambua: Nataka utuambie mapendekezao ungependa tufanye nini?

Com. Wambua: (Venacular) ...

Mzee Mboti: Hiyo shamba kama kawaida 1973, mtu akitakiwa kuchukua title deed apeliike shilingi 50/= au 100/= kwa survey office, apewe title deed. Haya ndio maoni yangu.

Com. Maranga: Jiandikishe hapo tafadhali. Asante sana Mzee Kivunza Mboti. Mrs. Roze Kioko.

Rose Kioko: I am Rose Kioko and these are my views on Constitution of Kenya Review Process.

(Interjection) Inaudible.

Local Government:-

Mayors and Council Chairmen should be elected directly by the electorates, they should not be in charge of a ward.

The 2-year term for Mayors and County Council Chairmen is inadequate instead it should be extended to 5 years.

They should be upright and ethically acceptable by the people e.g. they should not be criminals, not have been implicated in land grabbing or corrupt dealings.

I suggest that a Commission such as the Local Government Commission be formed to look into matters of remuneration

of Councillors.

Nominated Councillors should be retained, but should be morally and ethically upright people, of good educational status.

Women have not been well represented in the Local Governance. I therefore suggest that at least half representation of women be entrenched in the Constitution to ensure equity in governance of Local Authorities.

The Executive

In Kenya, Executive authority of the state is vested in the President but I recommend the following: -

That the Constitution should specify Presidential Candidates qualifications to be a University graduate, aged between 35 years and not more than 70 years of age.

He or she should be a Kenyan by birth and of sound mind.

He should also be a registered voter in any one of the electoral constituencies he or she wishes to contest in.

He should not have been declared bankrupt and must be a leader of a political party.

Presidential tenure should be 2 terms of 5 years each.

The Constitution should set limits on Presidential powers e.g. He or she should not prorogue Parliament, appoint and fire Senior Government Officials, he or she should not establish Commissions of inquiry instead, this should be done by Parliament.

The Constitution should provide for the removal of President for misconduct while in office through a Vote of No Confidence by Parliament.

We should have seats reserved for women and the disabled in Parliament to reduce the current disparities that exist in Kenya electoral system.

Our Constitutional provisions for fundamental rights are inadequate and should therefore also include right to access to clean water, clean environment, right to employment and right to gender equality.

The State should have the responsibility of ensuring that the all Kenyans enjoy basic rights like security, healthcare, education, water, shelter, food and employment.

The Constitution should provide for free and compulsory primary education for all Kenyans upto Standard 8.

The teachers who are curriculum implementers are not involved in fomulation of education policies, therefore they should be more involved and should have more say on matters of education.

The Current Constitution does not provide for the rights of groups of people who have suffered from marginalization due to historical, social, cultural or other reasons e.g. interest of women are not fully guaranteed in the Constitution and I suggest that they be addressed in the following ways:-

1. By passing laws protecting women e.g. Law to protect girls from being married at an early age.
2. By making provisions for affirmative action in favour of women, e.g. set a side a number of seats to be field by women in Parliament and Local Authorities.
3. Electing more women to Parliament and setting a side some posts in the sectors of the economy to be filled by women to allow participation in economic development at national level.
4. Allowing equal access to land by both men and women through passing a law to ensure that women also have a right to inherit land equally with men.

The Constitution should guarantee other basic rights like social security for the old, where the state should allocate a certain amount of money to take care of the old on attaining the age of 55 years.

Thank you.

Com. Maranga: Thank you Rose Kioko, there is a point of clarification from Commissioner Wambua.

Com. Wambua: You have mentioned the right to recall or impeach or pass a vote of no confidence on the President, if he does not perform. I did not hear you mention anything to do with a Member of Parliament or the Councilor. Can you say something about that? Do you say there even when they do not perform or do you have something to propose?

Rose Kioko: I wish to suggest that if a Councillor or a Member of Parliament does not perform or has some misconduct, he should be recalled by the electorate.

Com. Maranga: Thank you Rose Kioko please I want to request you to submit your memorandum and sign up our official register. Thank for your presentation, you move to the other side. The next person is Chief Musyimi, sorry it is Cliff Musyimi.

Cliff Musyimi: Asante sana Chairman, majina yangu kamili ni Cliff Mwicha Musyimi kutoka Matinyani Location.

Sana sana mimi nilikuwa nataka kuongea kuhusu corruption here in Kenya. Nikianza, kulingana vile naona, watu wanafikiria corruption inafanywa kuanzia chini, lakini kwa maoni yangu, naona corruption inaazia juu. Nitachukua mfano moja ya watu wa serikali kama Polisi. Hapa unaona Polisi ni mtu analipwa Shilling 7,000/= kwa mwezi na mtu ambaye ana familia, watoto wako shule na yeye mwenyewe anastahili kulisha hiyo familia, kuivalisha na kusomesha watoto.

Hiyo 7,000/=, ukipanga hiyo mshahara na Polisi, pengine mtu ako Mombasa au Nairobi na familia iko nyumbani hiyo mshahara haitoshi kabisa. Kwa hivyo naonelea sisi Wanakenya, Katiba iweze kufanya kazi, ili mtu yeyote hata ikiwa nani, wacha Polisi, iwe iko standing salary ya mfanyakazi yeyote, yule amejua ameandikwa na serikali kwa mfano kiwango kama 30,000/= yule ambaye ni wa kiwango ya chini, awe anafanya ama kazi yoyote, huyo ndio standanding salary yake. Kutoka hapo, mshahara ipandishwe kulingana na masomo ya mtu, kwa sababu mtu akipewa 4,000/= au 6,000/= atalipa nyumba, analisha watoto e.t.c. Hiyo pesa haitoshi ndio unaona ikitokea nafasi ya kuandikana mahali, utapata wale watu ambao wana pesa ndio watoto wao wanaandikwa kwa sababu wanapita kichinichini. Niandike huyu mtoto, na huyu mtoto labda hata masomo hajafikisha mahali, yule amewachwa nje, amefika.

Nitachukua mfano mwingine wa Minister. Minister anafanya kazi, wakati wowote amelindwa na Polisi, huyu Polisi anafanya kazi masaa 24 au 12 na unakuta Minister mwenyewe mahali popote wanaenda anakula na anakunywa, lakini Polisi mahali aliandikwa nje hajapata chochote. Mtu kama huyo unamtegemea afanye kazi vizuri kazi itawezekana kweli ikienda namna hiyo?

Kitu kingine ningependa kutaja ni juu ya hali ya usalama sana sana hapa kwetu Kitui. Hapa kwetu Kitui naona tuko na upunguvu wa ulindaji wa usalama, kwa sababu kitu ikitendeka hapa, mahali pa kukimbilia karibu ni Kitui, ni kutoka Kitui mpaka Kabati, ukiangalia area hii ya mlimani hakuna usaidizi pande huu ni Kitui tu. Tungeomba Katiba iweze kuongea na serikali tuwekewe Police Post humu kwetu ndani, ndio kitu ikitendeka tunakimbia haraka ili tusaidiane.

Maoni yangu yamefika hapo.

Com. Maranga: Asante, inaonekana kuna swali kutoka kwa Commissioner Wambua.

Com. Wambua: Mapendekezo yake ingekuwa tuweke Police Post kwa Location, kwa Division kwa Village au namnagani? Tunataka proposal ambayo iko specific.

Cliff Musyimi: Nilikuwa naonelea, Police Post ziwe katika Divisions, kama hapa Matinyani tuwe na Police Post hapa karibu.

Com. Maranga: Asante Bwana Musyimi, sasa nakuomba uweke sahihi kitabu chetu rasmi. Mwingine nitamwita sasa ni Munyoki Musee.

Munyoki Musee: Nimeshukuru Mwenyekiti. Maoni yangu si mengi sana, Jina langu ni Fredrick Mynyoki Musee kutoka hapa Matinyani.

Ningependekeza ya kwamba tunapoingia katika uchaguzi, tunapomchagua Rias, vile vile tumchague Makamu wake.

Wadhifa wa Rais upunguzwe kama, tunasikia Rias ndiye anachagua Makamu wake, na Rais huwa anachagua yule anampendeza, kwa hivyo ningependekeza tunapoingia kwa uchaguzi, tumchague ata Makamu wa Rais kupitia kwa kura.

Napendekeza ya kwamba tunapoingia shugulu za uandikishaji wa kura au kuesabiwa kwa watu ama kitu kama hicho. Kabla hizo shuguli hazijaanza, watu waelimishwe, wapewe civic education kwanza, kabla ya hayo mambo. Ningependekeza hiyo iwekwe kama sheria.

Vile vile ningependekeza ya kwamba, top government officials, kwa wakati moja, unasikia huyu ndiye Permanent Secretary tena ndiye Chairman wa Corporation fulani kwa hivyo ningependekeza one man one job. Mtu awe na kazi moja tu.

Ningependekeza vile vile, top Government Official after a certain period to declare their wealth. Wawe wakitambua mali yao yote na vile wamepata hiyo mali, hiyo itakuwa njia moja ya kupampana na ufisadi. Tukiangalia nchi zile ambazo zimeendelea kam Denmark, utapata kwamba baada ya muda fulani, watu wale wanashukilia nyadhifa kubwa katika serikali wana-declare their wealth.

Maoni yangu si mengi ni hayo tu.

Com. Maranga: Asante Bwana Musee. Kuna swali? No. Thank you very much, sign our official register. Asante sana, the next one is Munyalo Kieti. Wakati ni wako Mzee wangu, kuja moja kwa moja.

Munyalo Kieti: Jina langu ni Munyalo Kieti kutoka Matinyani Location, Kiondoni Sub-Location. Maoni yangu si mengi ni machache.

Mimi napendekeza Katiba ikitengenezwa sikukataa watu wa serikali wafanye biashara lakini maoni yangu hasa ni kwa Ministers. Nitatoa sababu ya Minister kukosa kufanya biashara. Minister ndiye anatengeneza Cabinet, ndio wanajua vitu vile vinaongezeka na yeye mwenyewe wakati wanaongeza bei za vitu, maanake ndio wanakaa katika Cabinet, wakijua bidhaa ambazo zimeongezwa bei, siku hiyo nafikiri Minister hawezi kulala. Atasema kitu fulani ipishwe, na kwa kweli kabla ya budget kusomwa hiyo bidhaa inapotea, na wakati budget inasomwa, utaona bidhaa ni nyingi zinatoka. Je, ikiwa mkebe ya Kimbo imeongezeke Shillingi moja na anapitisha Kimbo Million 20, akitoa anatajirika anatajirika nakuwa Millionaire. Kwa hivyo ile nataka Katiba ikitengenezwe wacha watu wa serikali, Minister ndio wako ndani ya Cabinet ambayo inaongeza bei za bidhaa na harusiwi kujua, hiyo ni siri ya serikali haitakikani kujulikana.

Mimi Bwana Chairman nasema ikiwa Katiba itatengenezwa, Minister afanye biashara akitoka katika bunge. Maanake ndio wanatengeneza kila kitu katika Cabinet halafu ananyanyasa wananchi kwa kupoteza bidhaa na baada ya kusoma budget, bidhaa zinatoka

La pili, nataka katiba ikitengenezwa, sisi wazee wale tume-retire hatufikiriwi, serikali ikiongeze watu mshara, kale kamshahara yangu ya pension haiongezwi na bei ya bidhaa inaongezeka. Nataka mkitemeneza Katiba, sisi wazee tuangaliwe serikali ikiongeza pesa, ili sisi pia tuongezewe kitu kidogo. Tume kaa pale, pale na mambo yanazidi kuongezeka na sisi hatungezewi.

(Interjection)

Ya nne nataka kuomba serikali ikitengeneza sheria, vile watoto wa mtaa wamekuwa wengi sana na mimi nashangaa vile wanakuwa wengi. Siku hizi boss ama hawa wakubwa wanazaa na watoto wa watu. Akishazaa, mtoto anawachwa hivyo, mama hana nguvu, na hiyo nyumbani hao ni maskini, mtoto anakosa malezi, halafu wanakwenda town. Wakitaka kupunguza “chokora” au watoto wa mtaani, yule yule amezaa na huyo mtoto alazimishwe kulea huyo mtoto kabisa maanake wale wanazaa hao watoto ni watu wale wako na mali. Akishafanya mapenzi na mtoto wa mtu, anamwacha hivyo na mama yake huyo mtoto ni maskini. Huyo boss amemaliza haja yake.

Katiba ikitengenezwa iangalie kabisa, yule amezaa naye alazimishwe kulea huyo mtoto na hatutaona “machokora” wakiwa wengi katika town. Maanake wanatokana na wasichana wale wanazaa watoto na hao watoto wanakosa pa kuenda, mwenye kuzaa na huyu arusiwe kulea mtoto. Nafika hapo.

Com. Maranga: Asante Mzee Kieti, inaonekana kuna swali kutoka kwa Commissioner Ayonga.

Com. Pastor Ayonga: Mzee Kieti, Je, itakuwaje kwa mtu aliekuwa anafanya biashara na ndipo amekwenda bunge, biashara bado iko, ilikuweco, huyu mtu atafanywa je? Pengine nadhani mawazo yako yalikuwa kwa watu wale ambao wanaingia bunge

ndipo wanaanza biashara. Lakini utamfanyaje mtu alikuwa anafanya biashara na amekuwa Minister? Hiyo hukutuambia.

Mzee Kieti: Sababu yake, kusema hivi mimi najua, ni kujua siri za zile vitu wanatengeneza wakiwa kwa Cabinet na anajua siri.

(Interjection)

Com. Ayonga: Wanajua siri?

Mzee Kieti: Wanajua siri za vile vitu ambazo zinaongezeka, yote wanapitisha, maanake ndio wako katika biashara. Wakati budget inasomwa, kila kitu inatoka, inaanza kuwa nyingi.

Com. Ayonga: Lakini hujaniambia, tumfanyeje huyu mtu. Tuseme huyu mtu alikuwa mwenye biashara ya petroli na ameenda Parliament, sasa atawacha hiyo biashara yake?

Mzee Kieti: Hatawacha hiyo biashara yake, isipokuwa yaangaliwe njia gani inaweza ku

Com. Ayonga: Hiyo njia ndio tunataka kutoka kwako?

Mzee Kieti: Hiyo njia ndio mnataka?

Com. Ayonga: Ndio, hayo ndio maoni yako, sisi hatuendi kuangalia, sisi tumekuja kuchukua maoni yako na ndio tunataka utuambie?

Mzee Kieti: Sasa mimi nimefika hapo maanake siwezi kueleza.

Com. Maranga: Asante Mzee Munyalo Kieti, sasa nakuomba uje uweke sahihi kitabu chetu rasmi. Asante sana.

Mzee Kieti: Nimejibu yote yale maswali yote mmeuliza.

Com. Maranga: Iko sawa sasa. Kuja uweke sahihi. Yule anayefuata anaitwa Boniface Bunyo au Bungo, atatuambia.

Boniface Masuu Kavungo: Habari ya Commissioners. Ningependa kutoa pendekezo langu. Ninaitwa Boniface Masuu Kavungo.

1. Mwanzo, nataka kutoa pendekezo langu kuusu elimu ya viongozi. Katiba ya Kenya ningetaka isiweke vikwazo kuusiana na

viongozi kuusu elimu maanake kuna viongozi ambao wanahitajika waongoze watu lakini hawana elimu na ndio wanafaa. For example, unaweza kumchukua mtu kama Councilor ambaye ni wa Form 4 na hawezi kujua kukaa na watu halafu upate mwingine ambaye hajafika hata Standard 2 na anajua kuishi na watu, hiyo inamaanisha viongozi wanahitajika wale ambao wanajua mwenendo wa watu.

2. Viongozi watakoachaguliwa walindwe, kwa sababu kuna uwezekano ya kuwa kiongozi ni mzuri na kwa vile kuna watu wanamwandama sana, uongozi wake uandamwa na wale na serikali ingilie na mwisho kabisa kiongozi aliyekuwa anahitajika na watu atupuliwe mbali, halafu kunaletwa mtu mwingine ambaye hawezi ule uongozi.

3. Elimu: Elimu hapa nchini Kenya imeanza kuzorota sana. Inamaanisha walioelimika kitambo ndio wataendelea na kuwa wameelimika kwa sababu mwanzo, kunashida sana katika sehemu zingine hapa nchini. For example kama Ukambani utakuta kuna watu ambao hawana mapato ya juu na wanaendelea na kuzaa na ile hali ya kuelimisha watoto wanashindwa. Unakuta katika familia, kuna mtoto mmoja ambaye elimu yake ama kuzaliwa kwake unastahili kumwezesha kusoma hata mpaka elimu ya hali ya juu sana lakini kulingana na ukosefu wa mapato na vile area yao iko remote au wazazi wako hawana chochote unakuta hakuna mtu anayetumia maanani. Kwa hivyo katika elimu ya watu ambao hawajiwezi, itiliwe manani sana, na serikali ijayo kupitia Katiba ya Kenya ichukue hatua kwa wazazi kama wale ambao wako na wale watoto. Kuzaa mtoto sio makosa bali kumelimisha na kumlea ndio shida kabisa.

4. Hospitali: Serikali hapa nchini Kenya ni lazima itilie maanani kuhusiana na ugonjwa unaopitia kwa watu kila wakata. For example unakuta hapa nchini Kenya kuna hospitali na hii hospitali sio mtu binafsi alitengeneza na wakati aliajiriwa kule na serikali na anapata pesa ya kumridhishia mambo yake yote, unakuta pale kwenye hospitali amefungua hospitali ingine pale ndani na ametoka nje kuenda kufungua hospitali ingine. Kwa hivyo ningepomba serikali na Katiba mpya impunguzie wafanyikazi wa serikali kuwa na biashara ya hospitali nje ya hospitali. Wafanye kazi ya hospitali peke yake na waridhike na ile mshahara wanapata pale.

Kwa hivyo mtu yeyote atakayeusika na hospitali za nje, hiyo biashara yake na lincence zake zifutuliwa mbali.

5. Ningeomba Katiba mpya iwe inashugulikia sana areas zile remote sana e.g. Ukambani, Umasaini, Turkana areas kama hizo, sababu gani? Kuna shida ya stima, kuna shida ya maji na kuna shida ya barabara. Serikali isahau areas zile zimeendelea sana na iangalie wenye shida.

For example areas kama Ukambani, wakati wa mvua nyingi unakuta mito nyingi hazivukwi kwa sababu hakuna bridge, zilizengwa chini ya mto sasa huwezi kusema kwamba uko Kenya na hali ni mbaya.

6. Masharti magumu ya kufanya kazi hapa nchini ama nchi za nje. Ningeomba Katiba mpya ituruhusu vijana wale tumekosa

kazi hapa kutokuwa na masharti magumu ya mtu akipata kazi nje ya nchi uwa anawekewe vikwazo. Kama kitu kama Passport Mkenya mwenyewe anapewa Passport bila masharti yeyote, kwa sababu ametafuta kazi nchini na hakuna. Kwa hivyo tuurusiwe uwa tunatoka nje bila kuwa na masharti hayo magumu.

7. Vijana wa Kenya wamekaa siku nyingi bila kazi, na ukiangalia percentage nyingi ya vijana wa hapa nchini wamekaa bila kazi.

